TANGAZO LA SERIKALI NA. 516 la tarehe 21/6/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahutaji vinginevyo:

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria au mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa baiskeli, mkokoteni au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi

inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni eneo liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kwa ajili ya kutolea huduma na biashara za mazao na bidhaa mbalimbali;

Sura ya 167

"hifadhi ya barabara" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Barabara;

"kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa huduma" maana yake ni ushuru unaotozwa au unaokusanywa na Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara au mfanyabiashara kwa huduma anazopata kutokana na kutumia miundombinu ya umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii;

"mwalo" maana yake ni miundombinu ya wachimbaji wadogo wa kukamatia dhahabu kwa kutumia madini ya zebaki ambao umejengwa kwa saruji, kuzungushiwa mfereji wenye nailoni na kuwekewa uzio madhubuti ili kuzuia uchafuzi wa

mazingira;

"mtambo wa kuchenjulia mabaki ya mchanga kwa kemikali" au "*vat leaching plant*" maana yake ni mtambo unaotumika kuchejua mabaki ya mchanga yanayosadikika kuwa na dhahabu kwa kutumia kemikali aina ya sianidi baada ya mabaki hayo kuchenjuliwa na zebaki;

"tani moja ya mazao mchanganyiko" maana yake ni ujazo wa gunia kumi za mazao mchanganyiko wenye uzito usiozidi kilo tisini kila moja au ujazo wa kuanzia gunia kumi za mazao ambazo kila gunia halizidi ujazo wa debe sita.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali au leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama kwa viwango vilivyoilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo (1), uUshuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), aAda zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kwa wakati.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Afisa

Mwidhiniwa au Wakala, kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ukusanyaji wa madeni

7.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa

uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

8.-(1) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

9. Bila kuathiri masharti negine ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

10. Mtu anatenda kosa endapo-

(a) anashindwa, anadharau, anakwepa au anakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) anamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) anamzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) anatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa

ada au ushuru ndani ya Halmashauri;

(e) anatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri; au

(f) anatumia chombo chochote kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

Adhabu

11. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa lolote kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS. Na. 603 Mwaka 2015

13. Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe Mwaka 2015 inafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA
USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO

| Na | Aina ya zao | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Viazi | 3% ya bei ya kununulia. |
| 2. | Kabichi | 3% ya bei ya kununulia. |
| 3. | Karoti | 3% ya bei ya kununulia. |
| 4. | Matunda | 3% ya bei ya kununulia. |
| 5. | Vitunguu maji | 3% ya bei ya kununulia. |
| 6. | Nyanya | 3% ya bei ya kununulia. |
| 7. | Mchele | 3% ya bei ya kununulia. |
| 8. | Mahindi/alizeti/mtama/mpunga | 3% ya bei ya kununulia. |
| 9. | Pamba/tumbaku | 3% ya bei ya kununulia. |
| 10. | zao jingine lolote litakalolimwa na kuuzwa katika mamlaka ya Halmashauri | 3% ya bei ya kununulia. |
| 11 | Kibali cha kununua mazao | Tshs 100,000/= kwa Mwaka |

SEHEMU YA PILI
ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI

| Na. | Chombo cha Usafiri | Ada ya Usajiri kwa Mwaka |
|---|---|---|
| 1. | Pikipiki | 17,000/= |
| 2. | Bajaji | 22,000/= |
| 3. | Taksi/Pick up/mabasi madogo chini ya abiria 25 | 30,000/= |
| 4. | Mabasi makubwa au lori | 80,000/= |
| 5. | Mitambo ya ujenzi (trekta, katapila, n.k) | 50,000/= |

SEHEMU YA TATU
USHURU WA MAEGESHO KWA MAENEO
YALIYOTENGWA KWA AJILI YA MAEGESHO YA VYOMBO VYA USAFIRI AU BIASHARA.

| Na. | Chombo cha Usafiri | Kiasi kwa siku |
|---|---|---|
| 1. | Pikipiki | 300/= |
| 2. | Bajaji | 500/= |
| 3. | Taksi | 500/= |
| 4. | Lori chini ya tani 7/pick up/basi dogo | 3,000/= |
| 5. | Lori zaidi ya tani 7/basi kubwa | 4000/= |
| 6. | Ushuru wa kituo cha mabasi<br>Mabasi makubwa zaidi ya abiria 25<br>Mabasi madogo chini ya abiria 25 | <br>2000/=<br>1000/= |
| 7. | Magari mengine yasiyo ya biashara | 500/= |

SEHEMU YA NNE

ADA NA USHURU WA KULAZA VYOMBO VYA USAFIRI MAENEO YALIYOTENGWA NA HALMASHAURI

| Na. | Aina ya chombo cha usafiri | Kiasi kwa Siku |
|---|---|---|
| 1. | Gari (lori kubwa la mizigo) | 5,000/= |
| 2. | Fuso, kenta au magari mengoine ya mizigo | 3,000/= |
| 3. | Basi kubwa | 3,000/= |
| 4. | Teksi | 1,000/= |
| 6. | Magari binafsi yasiyo ya biashara | 1,000/= |

SEHEMU YA TANO

ADA YA VIBALI VYA SHEREHE, MATANGAZO, BURUDANI NA SHUGHULI ZA UTAMADUNI.

| Na. | Aina ya huduma | Kiasi cha malipo |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha ngoma za jadi | 20,000/=kwa siku |
| 2. | Mnada wa bidhaa | 10,000/=kwa siku |
| 3. | Mshereheshaji (MC) | 10,000/=kwa siku |
| 4. | Mapambo | 20,000/=kwa siku |
| 5. | Wapishi katika sherehe | 20,000/=kwa siku |
| 6. | Kibali cha kuchezesha maonesho,disko,bendi na sanaa za maonesho | Kijijini 20,000/=kwa siku<br>Mjini 50,000/=kwa siku |
| 7. | Kibali cha kuchezesha michezo ya kubahatisha | 300,000/= kwa kibali kwa mwaka |
| 8. | Kibali cha matangazo ya biashara | 10,000/= kwa tangazo |
| 9. | Mechi za mpira uwanja wa Halmashauri | 10% ya mapato ya kila mechi |
| 10. | Michezo ya pool/fete | 10,000/= kwa mwezi |
| 11. | Michezo ya korokoro | 20,000/= kwa mwezi |
| 12. | Kibali cha mechi za mpira | 10,000/=kwa kila mechi |
| 13. | Mazingaombwe | 5,000/= kwa siku mija |
| 14. | Ada ya usajili wa vikundi vya Sanaa | 25% ya usajili wa gharama za usajili BASATA |
| 15. | Ada ya usajili na vibali vya kumbi za burudani | 25% ya usajili wa gharama za usajili BASATA |
| 16. | Usajili na vibali vya vyama au vilabu vya michezo | 25% ya usajili wa gharama za usajili BASATA |

SEHEMU YA SITA

ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

| Namba | Aina ya mfugo | Kiasi kwa kila mmoja |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 4,000/= |
| 2. | Ada ya ukaguzi kwa ng'ombe aliyechinjwa | 3,000/= |
| 3. | Ada ya uchinjaji/machinjio kwa kila kondoo/mbuzi atakayechinjwa | 1,500/= |
| 4. | Ada ya ukaguzi ka kila kondoo/mbuzi atakayechinjwa | 1,500/= |
| 5. | Mifugo mingine | 2000/= |
| 6. | Ada ya ukaguzi kwamifugo mingine | 2,000/= |
| 7. | Ushuru wa bucha la ng'ombe, kondoo, nguruwe na samaki | 500/= |
| 8. | Ushuru wa ngozi ya ng'ombe | 300/= |
| 9. | Ushuruwa kulaza ng'ombe machinjioni | 1,000/=kwa siku kwa kila mmoja |
| 10. | Ushuru wa kulaza mbuzi/kondoo machinjioni | 500/=kwa siku kwa kila mmoja |
| 11. | Ada ya ukaguzi wa gari ya kubebea nyama | 50,000/=kwa Mwaka |

SEHEMU YA SABA

ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

| Na. | Huduma | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya pango la vibanda/vizimba vya biashara | Tozo itatajwa kwenye mkataba |
| 2. | Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya vikao, mikutano na sherehe | Tozo itatajwa kwenye mkataba |
| 3. | Kukodi viti vya Halmashauri | Tozo itatajwa kwenye mkataba |
| 4. | Mitambo (trekta, Total station, vifaa vya GPS na n,k) | Tozo itatajwa kwenye mkataba |
| 5. | Kukodi vipaza sauti na matarumbeta | Tozo itatajwa kwenye mkataba |
| 6. | Kutumia uwanja wa michezo kwa shughuli za biashara | Tozo itatajwa kwenye mkataba |
| 7. | Kusoma nyaraka za wazi za Halmashauri | Tozo itatajwa kwenye mkataba |
| 8. | Kutumia maktaba ya Halmashari | Tozo itatajwa kwenye mkataba |
| 9. | Mali nyingine ya Halmashauri | Tozo itatajwa kwenye mkataba |

SEHEMU YA NANE

ADA YA UKAGUZI WA AFYA

| Namba | Huduma | Ada |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za starehe (baa, vilabu vya pombe za kienyeji, na nyumba ya kulala | 3,000/=kila baada ya miezi mitatu |

*Tangazo la Serikali Na. 516 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | wageni) | |
| 2. | Nyumba ya kutengeneza na kuuzoia vyakula au nyama choma | 3,000/=kila baada ya miezi mitatu |
| 3. | Ukaguzi wa viwanda vikubwa | 150,000/=kwa mwaka |
| 4. | Ukaguzi wa viwanda vya kati | 100,000/=kwa mwaka |
| 5. | Ukaguzi wa viwanda vidogo | 50,000/=kwa mwaka |
| 6. | Kusajiliwa na kupima afya kwa wahudumu wa kulala nyumba za wageni, vinyozi, katika saluni za kike/kiume, hoteli, migahawa, wauzaji wa bucha, zahanati, mama/baba lishe, wauza matuda, baa, glosari, pombe za kienyeji, wafanyakazi sehemu za kuokea mikate na wahudumu katika mashine za nafaka | 2,000/= kwa kila muhudumu kila baada ya miezi mitatu |
| 7. | Kupima afya wanaojiunga vyuo, jeshi | 1,000/= |
| 8. | Kupima afya kwa wanaotaka kuajiriwa | 5,000/= |

SEHEMU YA TISA
USHURU WA MINADA YA MIFUGO

| Na. | Ushuru wa mifugo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe/punda (bila kibali) | 4000/=kwa kila mmoja |
| 2. | Mbuzi/kondoo/nguruwe (bila kibali) | 1500/=kwa kila mmoja |
| 3. | Kuku/bata/kanga | 2000/=tenga la kuku kuanzia 10 hadi 50 |
| 4. | Kuku/bata/kanga | 5,000/=kuanzia 51 na kuendelea |
| 5. | Mifugo mingine | 2,000/= kwa kila mmoja |

SEHEMU YA KUMI
ADA YA KUOGESHA MIFUGO

| Na. | Aina ya mifugo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe/punda | 400/=kwa kila mmoja |
| 2. | Mbuzi/kondoo | 200/=kwa kila mmoja |
| 3. | Mifugo ya kufuga sio kwa chakula | 300/=kwa kila mmoja |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
USHURU WA BIDHAA NYINGINE ISIYO MIFUGO INAYOUZWA MINADA YA MIFUGO.

| Na. | Ushuru | Kiasi kwa siku |
|---|---|---|
| 1. | Wauzaji wa nguo/mitumba | 1,000/= |
| 2. | Mama lishe | 1,000/= |
| 3. | Wauzaji wa vinywaji | 2,000/= |
| 4. | Biashara ndogondogo | 300/= |
| 5. | Pombe za asili | 500/= |

*Tangazo la Serikali Na. 516 (Linaendelea)*

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
USHURU WA MAGULIO, MASOKO NA MINADA ISIYO YA MIFUGO

| Na. | Aina ya shughuli/bidhaa | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Banda la kuuzia kuku sokoni, gulioni na mnadani | 500/= kwa siku |
| 2. | Uuzaji wa pumba na maganda ya karanga | 500/=kwa tripu mkokoteni wa punda<br>5,000/= kwa tripu trekta/fuso<br>10,000/=kwa tripu malori makubwa |
| 3. | Ushuru wa samaki wakavu | 1,000/= kwa tenga |
| 4. | Ushuru wa samaki wabichi | 1,000/=kwa tenga |
| 5. | Ushuru wa dagaa | 1,000/=kwa tenga |

SEHEMU YA KUMI NA TATU
USHURU WA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA MAGULIO, MASOKO NA MINADA

| Na. | Aina ya gari | Kiasi kwa siku ya gulio au soko |
|---|---|---|
| 1. | Gari dogo la abiria | 1,000/= |
| 2. | Gari kubwa la abiria | 1,000/= |
| 3. | Gari la mizigo lisilozidi tani 3 | 1,000/= |
| 4. | Gari la mizigo linalozidi tani 3 | 2,000/= |
| 5. | Magari mengineyo | 3,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA NNE
USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na. | Uzito wa gari | Kiasi kwa kila safari |
|---|---|---|
| 1. | Tani 1-2 | 3,000/= |
| 2. | Tani 3-7 | 5,000/= |
| 3. | Kwa kila tani itakayoongezeka | 1,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA TANO
ADA YA UKAGUZI NA UMILIKI WA KUCHIMBA
MADINI YA UJENZI

| Na. | Ada ya Ukaguzi | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya ukaguzi wa eneo jipya linalokusudiwa kuchimbwa madini ujenzi | 30,000/= |
| 2. | Ada ya umiliki wa eneo la kuchimbwa madini ujenzi | 50,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA SITA
ADA YA MATANGAZO YA MABANGO.

| Na. | Aina ya matangazo | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|
| 1. | Mabango ya biashara yasiyong'aa (kwa kila futi moja ya mraba) | 15,000/= kwa mwaka |
| 2. | Mabango ya biashara yanayong'aa (kwa kila futi moja ya mraba) | 25,000/=kwa mwaka |
| 3. | Mabango ya biashara yasiyong'aa (yanayodumu kwa siku saba) | 3,000/=kwa kila futi moja |
| 4. | Mabango ya biashara yanayong'aa (yanayodumu hadi siku saba) | 4,500/=kwa kila futi moja |
| 5. | Mabango ya biashara yasiyong'aa (yanayodumu hadi siku thelathini) | 5,000/=kwa kila futi moja |
| 6. | Mabango ya biashara yanayong'aa (yanayodumu hadi siku thelathini) | 7,500/=kwa kila futi moja |

SEHEMU YA KUMI NA SABA
ADA YA VIBALI VYA UJENZI

| Na. | Ujenzi/upimaji wa;- | Kwa kila kibali |
|---|---|---|
| 1. | Ghorofa | 300,000/= |
| 2. | Nyumba ya biashara | 100/000/= |
| 3. | Nyumba ya makazi | 50,000/= |
| 4. | Kituo cha mafuta | 300,000/= |
| 5. | Majengo ya taasisi binafsi | 500,000/= |
| 6. | Maghala na bohari | 200,000/= |
| 7. | Nyumba ya biashara na makazi | 120,000/= |
| 8. | Kibali cha ujenzi wa Mnara wa simu | 1,500,000/=kwa mnara |
| 9. | Upimaji wa mashamba kwa ajili ya kutengeneza hati miliki | 250,000/=kwa ekari 1-5<br>300,000/= zaidi ya ekari 5 |

SEHEMU YA KUMI NA NANE
ADA YA MABADILIKO (ALTERATION) YA JENGO LILILOPO, UPIMAJI NA USAFISHAJI WA VIWANJA

| Na. | Aina ya jengo | Kiasi cha Ada kwa kila kibali |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya kuishi | 100,000/= |
| 2. | Nyumba ya biashara | 150,000/= |
| 3. | Ghorofa | 400,000/= |
| 4. | Kiwanda, bohari, ghala | 200,000/= |
| 5. | Ada ya kukagua kiwanja kidogo (High density) | 10,000/= |
| 6. | Ada ya kukagua kiwanja cha kati (medium density) | 20,000/= |
| 7. | Ada ya kukagua kiwanja kikubwa (low density) | 30,000/= |
| 8. | Ada ya kukagua kiwanja kikubwa zaidi (super | 40,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | low density) | |

SEHEMU YA KUMI NA TISA
USHURU WA MAZAO YA MISITU YA HALMASHAURI

| Na. | Aina ya zao | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Gunia la mkaa | Tsh. 1,000/= kwa gunia |
| 2. | Mauzo ya mkaa usiokua na kibali | Tsh. 15,000/= kwa gunia |
| 3. | Ushuru wa nguzo za miti ya kupanda | Tsh.500/= kwa kila nguzo |
| 4. | Mauzo ya nguzo zisizokua na kibali | Tsh. 3,000/= kwa kila nguzo |
| 5. | Magogo | Tshs 15,000/= kwa kila gogo |
| 6. | Fito mita moja ya ujazo | Tshs. 5,000/= kwa kila mita moja ya ujazo |
| 7. | Mabanzi | Tsh. 500/= kwa kila banzi |
| 8. | Kuni | Tsh. 6,500/= kwa kila mita za ujazo |
| 9. | Mbao za miti ya kupandwa | Tsh. 500/= kwa kila ubao mmoja |
| 10. | Samani | Tsh.2,000/= kwa kila kimoja |
| 11. | Ushuru wa gogo la kupandwa | Tsh.5,000/= kwa kila mti |
| 12. | Debe la asali | Tsh.3,000/= kwa kila debe |
| 13. | Nta | 5% ya bei ya kununulia kwa kilo |

SEHEMU YA ISHIRINI
ADA NA USHURU WA SHUGHULI ZA MADINI YANAYOSADIKIKA KUWA NA DHAHABU

| Na. | Aina ya shughuli | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Kusafirisha senga/marudio nje ya Wilaya | 100,000/= kwa kila senga/marudio |
| 2. | Ada ya umiliki wa plant, CIP,CIL, na Elution plant | 1,500,000/= |
| 3. | Ushuru wa mifuko ya mawe | 1,000/=kwa kila mfuko mmoja |
| 4. | Usafirishaji wa Carboni nje ya Wilaya | 2,000,000/=kwa msafirishaji |
| 5. | Ushuru wa mwalo | 10,000/=kwa mwezi kwa kila mwalo |
| 6. | Ushuru wa karasha | 10,000/=kwa mwezi kwa kila karasha |
| 7. | Usafirishaji wa mifuko ya Mawe nje ya Wilaya | 1500/=kwa kila mfuko |

SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA
MGODI/RUSH ZA UCHIMBAJI WA MADINI YA DHAHABU

| Na. | Idadi ya mifuko kwa kila duara | Idadi ya mifuko |
|---|---|---|
| 1. | 11-49 | 1 mfuko wa mawe |
| 2. | 50-99 | 2 mifuko ya mawe |
| 3. | 100-114 | 3 mifuko ya mawe |
| 4. | 115-148 | 4 mifuko ya mawe |
| 5. | 149-183 | 5 mifuko ya mawe |
| 6. | Idadi ya mifuko ambayo haikutajwa | Itatolewa kulingana na idadi kwa kufuata mtiririko wa hapo juu |

*Tangazo la Serikali Na. 516 (Linaendelea)*

SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI
ADA YA USAJILI WA VIKUNDI

| Na. | Aina ya kikundi | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Usajili wa vikundi (CBOs) | 30,000/= |

SEHEMU YA ISHIRINI NA TATU
ADA YA HUDUMA YA USAFI WA MAZINGIRA

| Na. | Aina | Kiasi cha Ada kwa Mwezi |
|---|---|---|
| 1 | Wafanyabiashara wa sokoni | Tsh.4,000/= |
| 2 | Kuzoa taka Majumbani na maeneo ya mijini kila nyumba | Tsh.2,000/= |
| 3 | Kuzoa taka jengo la soko la dhahabu kwa kila sonara mwenye jiko | Tsh.5,000/= |
| 4 | Kuzoa taka Taasisi za Umma | Tsh. 5,000/= |
| 5 | Kuzoa taka Taasisi binafisi | Tsh. 5,000/= |
| 6 | Kuzoa taka Kituo cha mafuta | Tsh. 5,000/= |
| 7 | Kuzoa taka Duka la dawa la jumla na rejareja | Tsh. 5,000/= |
| 8 | Kuzoa taka Duka la dawa la rejareja | Tsh. 4,000/= |
| 9 | Kuzoa taka Stationaries na duka la kuuza vitabu | Tsh. 4,000= |
| 10 | Kuzoa taka Duka la jumla na rejareja | Tsh. 4,000/= |
| 11 | Kuzoa taka Mgahawa | Tsh.4,000/= |
| 12 | Kuzoa taka Grocery na kioski | Tsh. 4,000/= |
| 13 | Kuzoa taka kwenye Bar | Tsh.5,000/= |
| 14 | Kuzoa taka Duka la kuuza samaki/nyama | Tsh. 5,000/= |
| 14 | Kuzoa taka Kumbi za mikutano/sherehe/krabu za usiku | Tsh. 5,000/= |
| 16 | Kuzoa taka Mashine za kukoboa nafaka/Ghala la kuhifadhia mazao | Tsh. 5,000/= |
| 17 | Kuzoa taka Kiwanda/Kampuni | Tsh. 6,000/= |
| 18 | Kuzoa taka /gereji/fendi seremala/kuchomelea | Tsh. 5,000/ |
| 19 | Kuzoa taka Fundi cherahani | Tsh. 4,000/= |
| 20 | Kuzoa taka Saluni ya Kike/Kiume | Tsh. 4,000/= |
| 21 | Biashara yoyote mnadani; wauzaji wa nguo za mitumba/mpya, mama lishe,wauzaji wa mazao mchanganyiko,wauzaji wa vinywaji, mafundi cherehani | Tsh. 1,000/= kwa kila siku ya mnada |
| 22 | Kuzoa taka Biashara yeyote ambayo haijatajwa hapo juu | Tsh. 5,000/= kwa mwezi |

SEHEMU YA ISHIRINI NA NNE
ADA YA HUDUMA ZA AFYA

| Na. | Aina ya huduma | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Huduma kwa mtu aliyezidi umri wa miaka mitano aliyejiunga na mfuko wa bima ya afya iliyoboreshwa iCHF | 30,000/=kwa watu sita kwa mwaka |

*Tangazo la Serikali Na. 516 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Huduma ya afya ya papo kwa papo zahanati/kituo cha afya/Hospitali ya Wilaya | Kiasi kulingana na huduma zilizotolewa |
| 3. | Ada ya Waganga wa tiba asilia | 50,000/= kwa mwaka |

SEHEMU YA ISHIRINI NA TANO
ADA NA USHURU MWINGINE

| Na. | Aina ya huduma | Kiasi cha Ada na Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Choo cha umma cha kulipia | 300/=kwa kila huduma |
| 2. | Kibali cha kufyatua matofali | 20,000/=kwa mwaka |
| 3. | Ushuru wa nyumba za kulala wageni | 10%ya bei ya chumba kwa siku |
| 4. | Leseni za vileo | 40,000/=kwa miezi 6 |
| 5. | Ada ya zabuni za huduma | 10,000/= kwa kila ombi |
| 6. | Ada ya zabuni za ujenzi | 150,000/= kwa mkandarasi<br>10,000/=kwa local fundi |
| 7. | Kuingia ndani ya stendi/ kituo cha mabasi kwa mtu asiyekua na tiketi | 200/=kwa siku |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Mbogwe, kwamba mnamo Tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Mwaka, 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……………....... ya Mwezi…………..…................... Mwaka …………….

Jina……………………………….......................... Saini……….......………………

*Tangazo la Serikali Na. 516 (Linaendelea)*

MBELE YANGU :
Jina:…………………………………..……………………
Saini………………………..………………………...………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe…………………………………………………………

Lakiri ya Halmashuri ya Wilaya ya Mbogwe imegongwa kwenye Sheria ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe uliofanyika tarehe10 Mwezi Juni Mwaka 2020 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikigongwa mbele ya;

SAADA SELEMANI MWARUKA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe*

VINCENT BENEDICTOR LUBAGA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe*

NAKUBALI,

**L.S**

Dodoma.
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Raisi*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa)*